



# JARIDA

LA MTANDAONI | TOLEO LA MACHI 2022

USHIRIKI WA NSSF KATIKA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA JUKWAA  
LA WAHARIRI TANZANIA



Tunajenga Maisha Yako  
ya Sasa na Baadaye

## NSSF

[www.nssf.or.tz](http://www.nssf.or.tz)

Simu Bure  0800116773  
[customercare@nssf.or.tz](mailto:customercare@nssf.or.tz)

@NssfTanzania





## Rais Dkt. Mwyni abainisha maeneo muhimu kuhusu uchumi wa buluu

\* TEF yaipongeza NSSF kwa kutoa msamaha wa tozo kwa waajiri wa sekta binafsi

### Na MWANDISHI WETU

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwyni amezindua mkutano mkuu wa mwaka wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) huku akibainisha maeneo matano muhimu kuhusu uchumi wa buluu ambao ndio sera na muelekeo wa Serikali anayoiongoza.

Akifungua mkutano huo katika ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul-Wakil mjini Zanzibar, Dkt. Mwyni alisema uchumi wa buluu una sekta tano kubwa ikiwemo utalii, uvuvi na ufugaji wa samaki, bandari, usafiri na biashara za baharini pamoja na mafuta na gesi.

Rais Dkt. Mwyni alisema hayo ndio maeneo muhimu katika kukuza na kuendeleza uchumi wa buluu ambapo alitumia fursa hiyo kulipongeza jukwaa la wahariri kwa uamuzi wake wa kuamua kufanya mkutano huo visiwani Zanzibar wenye kauli mbiu isemayo "Uchumi wa Buluu na Mawasiliano ya Umma.

Balile alisema NSSF inafanya mambo mengi mazuri hasa katika kuunga mkono juhudi mbalimbali za wadau pamoja na kutatua changamoto za wanachama ambapo Bodi ya Wadhamini ya Mfuko ilitoa msamaha wa tozo kwa waajiri waliokuwa na malimbikizo ya michango kwa muda wa miezi mitatu na kufanikiwa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 39 katika kipindi hicho.

Wakizunguma kwa nyakati tofauti, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape Nnauye na Waziri wa Habari wa Zanzibar, Mhe. Tabia Maulid Mwita alisema walipongeza juhudi kubwa zinazochukuliwa na TEF katika kuhabarisha umma kuhusiana na mafanikio mbalimbali ya Serikali.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi akimkabidhi cheti cha udhamini wa mkutano mkuu wa jukwaa la wahariri Tanzania, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhmini ya NSSF, Balozi Ali Iddi Siwa



Rais Dkt. Mwinyi akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali baada ya kuzindua mkutano mkuu wa mwaka wa jukwaa la wahariri Tanzania katika ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul-Wakil mjini Unguja

# NSSF yatoa semina katika mkutano mkuu wa mwaka wa jukwaa la wahariri Tanzania

Na MWANDISHI WETU

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umeshiriki katika mkutano mkuu wa mwaka wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) na kutoa semina kuhusu mambo mbalimbali yanayofanywa na Mfuko katika kustawisha sekta ya hifadhi ya jamii nchini pamoja na kueleza dhamira yake ya kukuza maendeleo endelevu ya Taifa.

Semina hiyo ilifanyika katika ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul-Wakil mjini Zanzibar, baada ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kufungua mkutano huo uliokuwa na kauli mbiu isemayo "Uchumi wa Buluu na Mawasiliano ya Umma".

Akizungumza katika semina hiyo Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba alisema kupitia mkutano huo Mfuko ulitoa semina kuhusu majukumu ya msingi ya Mfuko ambayo ni kuandikisha wanachama kutoka sekta rasmi na sekta isiyo rasmi, kukusanya michango, kuwekeza na kulipa mafao.

Mshomba alisema Mfuko umedhamini mkutano huo kwa kutambua umuhimu wa jukwaa hilo hasa ukizingatia kuwa ulitumia mkutano huo kuwajengea uelewa wahariri hao wa vyombo vya habari kuhusu umuhimu wa hifadhi ya jamii kwa maisha ya sasa na baadaye.

Akitoa mada kuhusu shughuli zinazofanywa na Mfuko, Meneja wa Usimamizi Mafao wa NSSF, James Oigo aliwaeleza wajumbe wa mkutano huo dhana ya hifadhi ya jamii pamoja na majukumu na muundo wa NSSF ambapo alibainisha kuwa Mfuko umesogeza huduma zake karibu na wanachama kupitia mifumo ya Tehama.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile alipongeza kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Mfuko hasa katika kufikisha elimu ya hifadhi ya jamii kwa Watanzania waliojiajiri kupitia sekta rasmi na sekta isiyo rasmi wakiwemo wakulima, wavuvi, wafugaji, mama lishe, bodaboda na wajasiriamali wengine.



Meneja Usimamizi wa Mafao NSSF, James Oigo akitoa mada kuhusu shughuli zinazofanywa na Mfuko wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa Jukwaa la Wahariri Tanzania







**Tunajenga Maisha Yako  
ya Sasa na Baadaye**